



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
WAKALA WA CHUO CHA TAIFA CHA UTALII  
Shaban Robert/Samora Street

S. L. P. 9181  
Dar es Salaam  
TANZANIA  
[www.nct.ac.tz](http://www.nct.ac.tz)

Simu: 0738274574  
Fax: 255 22 2125248  
E-mail: [principal@nct.ac.tz](mailto:principal@nct.ac.tz)



## TAARIFA KWA UMMA

Mkuu wa Chuo Cha Taifa Cha Utalii (NCT) anayofuraha kuwatangazia wananchi na wadau wote kuwa Chuo Cha Taifa Cha Utalii Kampasi ya Arusha kimepata fursa ya kutoa mafunzo ya Uanagenzi chini ya Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini inayolenga kuwezesha nguvu kazi ya Taifa kupata ujuzi na stadi za kazi stahiki ili kumudu ushindani katika soko la ajira. Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu. Kwa awamu ya Saba (7) Chuo kimepata fursa ya kutoa mafunzo kwa fani ya Mapishi (Culinary Arts), Huduma ya Chakula na Vinywaji (Food and Beverage Services), Mapokezi (Front Office Operations), Huduma za Ndani na Utunzaji wa vyumba vya wageni (Housekeeping and Laundry), Shughuli za Usafirishaji na Utalii (Travel and Tourism), Uongozaji wa Watalii (Tour Guiding Operations), Upishi na Uokaji wa Mikate na keki (Pastry and Bakery). Mafunzo hayo yanatarajiwa kuanza tarehe **03 Machi, 2025**. Gharama zote za Mafunzo haya zitagharamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu na mzazi/mwanafunzi atagharimia malazi, nauli na chakula.

Chuo kinawakaribisha waombaji wote wanaopenda kunufaika na program hiyo ya mafunzo kuomba kwa kujaza fomu ya maombi kabla ya terehe 12.02.2025. Fomu za maombi zinapatikana kwenye tovuti ya Chuo kupitia kiunganishi [www.nct.ac.tz](http://www.nct.ac.tz) au wasiliana na mratibu kwa namba 0738274574 au fika Ofisi ya Kampasi yoyote ya Chuo cha Taifa cha Utalii Jijini Arusha, Dar Es Salaam na Mwanza. Sifa za kujiunga na mafunzo haya ni:

- i. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- ii. Awe Mtanzania;
- iii. Awe na umri kati ya miaka 15 – 35; na
- iv. Awe mwenye afya njema.

Maombi hayo yaambatanishwe na nyaraka zifuatazo; -

- i. Barua ya maombi ya mafunzo;
- ii. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa;
- iii. Nakala ya Cheti cha elimu uliyohitimu;
- iv. Kitambulisho cha uraia / kadi ya mpiga kura (Kwa wenye miaka 18 na kuendelea);
- v. Barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Serikali ya Mtaa/Kijiji anakoishi mwombaji;
- vi. Picha nne za paspoti (ziandikwe majina matatu ya mwombaji kwa nyuma).

IMETOLEWA NA:  
OFISI YA MKUU WA CHUO  
01/02/2025